



## 1.0 UTANGULIZI

### a) LENGU LA MFUKO

Kuinua ubora wa kazi za Utamaduni na Sanaa ili ziweze kujiendesha kibiashara na kutengeneza ajira nchini.

### b) SEKTA ZINAZOHUJUMIWA NA MFUKO

Muziki, Filamu, Sanaa za Ufundi, Sanaa za Maonesho, Lugha na Fasihi

### c) WALENGWA WA MFUKO

Mtu binafsi, Kikundi, na Kampuni

## 2.0 HUDUMA ZA MFUKO

### a) MIKOPO

Ununuzi wa vifaa, Uendeshaji, Dharura/Kujikimu

### b) MAFUNZO

Kuwajengea uwezo wadau wa Utamaduni na Sanaa.

## 3.0 VIGEZO VYA KUOMBA MKOPO

- Mwombaji awe raia wa Tanzania.
- Awasilishe andiko la mradi linalobainisha malengo mahsusi ya mkopo na mchanganuo wa namna atakavyorejesha mkopo husika.
- Awasilishe uthibitisho wa uhai wa usajili kutoka Taasisi inayosimamia utekelezaji wa majukumu ya mwombaji kwenye Sekta ya Utamaduni na Sanaa.
- Awasilishe uthibitisho kuwa ni mwanachama wa Umoja wowote ikiwamo Shirikisho, Chama au Kikundi kilichosajiliwa kisheria katika Sekta ya Utamaduni na Sanaa na ametambulishwa kwa maandishi na umoja huo.
- Kwa waombaji wa vifaa: Iwasilishwe Ankara kifani (invoice) kutoka kwa muuzaji anayetambulika. Ankara kifani ionyeshe aina, na thamani ya kifaa kazi kinachohitajika.
- Awasilishe barua ya utambulisho kutoka serikali ya Mtaa/Kijiji mahali ambapo mradi unafanyika.
- Awasilishe barua ya utambulisho kutoka serikali ya Mtaa/Kijiji mahali anapoishi

## 4.0 SIFA ZA MIKOPO

- Kiwango cha mikopo ya kawaida ni kuanzia TZS 200,000/= hadi TZS 100,000,000/=
- Muda wa marejesho ni miezi 24 (Miaka 2)
- Riba ni asilimia tisa (9%) inayotozwa katika salio la mkopo
- Muda wa rehema (grace period) ni miezi mitatu (3)

### Maombi yote yatumwe kwa:

Afisa Mtendaji Mkuu,  
Mfuko wa Utamaduni na Sanaa,  
S.L.P 8031,  
**DAR ES SALAAM.**

### Na kuwasilisha kupitia:

Barua pepe: [mfuko.utamaduni@michezo.go.tz](mailto:mfuko.utamaduni@michezo.go.tz)  
**Au**  
Ofisi za Mfuko zilizopo:  
Jengo la Utumishi,  
Block A, 8 Barabara ya Kivukoni,  
11101 Kivukoni, Dar es salaam.